## Maswali

1. Mbona Wakristo wengi waliondoka Yerusalemu?
2. Filipo aliende kuishi wapi?
3. Filipo alifanya nini kwa mji wa Samaria?
4. Watu waliokuwa wamebatizwa walipewa nini na Petro na Yohana?
5. Simoni alitaka kununua nini? Petro na Yohana walisema nini?
6. Filipo alikutana na nani kwa barabara ya jangwani?
7. Mkushi alikuwa anasoma nini?
8. Filipo alifundisha Mkushi nini?
9. Mkushi alitaka kufanya nini alipoona maji?
10. Filipo alibatiza Mkushi namna gani?

## Majibu

1. Wakristo wengi waliondoka Yerusalemu kwa sababu walikuwa wanateswa.
2. Filipo aliende kuishi kwa mji wa Samaria.
3. Filipo alifundisha watu juu ya Yesu. Aliponya watu wagonjwa wengi.
4. Petro na Yohana waliwapea nguvu za Roho Mtakatifu.
5. Simoni alitaka kununua nguvu za Roho Mtakatifu ili auzie wengine. Petro alimwambia kwamba nguvu za Mungu haziwezi kununuliwa. Ilikuwa ni vibaya sana kupata pesa kwa kutumia nguvu za Mungu.
6. Filipo alikutana na Mkushi. Alikuwa mweka hazina wa Malkia wa Kushi.
7. Alikuwa anasoma chuo. Alikuwa anasoma Isaya mlango wa 53.
8. Filipo alimfundisha juu ya Yesu na Ufalme wa Mungu.
9. Mkushi alipoona maji alitaka kubatizwa.
10. Filipo alitelemsha Mkushi ndani ya maji. Alimwinamisha mpaka ndani ya maji.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 2

# 92 Filipo

### Kwa Biblia

Matendo ya Mitume mlango wa 8

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mkushi alitakiwa aelewe Habari Njema ya Yesu Kristo na Ufalme wa Mungu kabla ya kubatizwa. Filipo alimbatiza kwa kumzika ndani ya maji.

### Somo

Wakristo waliokuwa Yerusalemu waliteswa. Wakristo wengi waliondoka Yerusalemu. Walienda kuishi kwa miji mingine. Filipo aliende kuishi kwa mji wa Samaria. Filipo alifundisha watu juu ya Yesu. Aliponya watu wengi. Watu wa huo mji walifurahi sana kwa sababu marafiki na jamii wao wengi waliponywa. Wengi wao walikuwa na imini kwa Yesu. Waliuliza Filipo awabatize.

Kulikuwa na mtu mmoja jina lake Simoni aliyeishi kwa huo mji. Alifanya uchawi mwingi akidanganya watu kwa uchanja. Huyu Simoni aliamini mafundisho ya Filipo juu ya Yesu. Alibatizwa. Simoni alishangaa sana kwa ajili ya miujiza yenye Filipo alifanya kutumia nguvu za Roho Mtakatifu.

Petro na Yohana walienda kumwona Filipo. Walifurahi kuona kwamba watu wengi waliamini kwa Yesu na wakabatizwa. Petro na Yohana waliwapa wale watu waliobatizwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Na wale watu nao waliweza kufanya miujiza.

Simoni aliona Petro na Yohana wakipea watu nguvu za Roho Mtakatifu. Simoni aliona kwamba anaweza kupata pesa nyingi sana kama angeweza kupeana nguvu za Roho Mtakatifu. Simoni alifikiria vile angekuwa tajiri kwa kuuzia watu nguvu za Roho Mtakatifu.

Simoni alimpa Petro na Yohana pesa. Aliwauliza wamuuzie kipawa cha nguvu za Roho Mtakatifu ili awape watu. Petro alikasirika sana. Alijua Simoni alitaka kutumia nguvu za Mungu kukuwa tajiri. Petro alimwambia Simoni, "Hauwezi kununua nguvu za Mungu kwa pesa. Mungu hauzi vibawa vyake kwa mtu yeyote. Mungu hupeana kipawa kwa mtu anayempenda. Lazima uombe na uulize Mungu akusamehe kwa hayo mawazo maovu."

Malaika aliambia Filipo asafiri kusini kuelekea jangwani. Filipo alianza safari. Njiani alikutana na mwanamme Mkushi. Huyo Mkushi alikuwa mtu wa maana sana. Alikuwa mweka hazina wa Malkia wa Kushi. Huyu Mkushi alikuwa ameenda Yerusalemu kuabudu Mungu. Alikuwa kwa gari anarudi nyumbani Kushi.

Mkushi alikuwa anapumzika juu ya gari. Alikuwa anasoma chuo kutoka Agano la Kale. Roho Mtakatifu alimwambia Filipo aende azungumze na huyo mtu.



Huyo Mkushi alikuwa anasoma kwa kitabu cha Isaya mlango wa 53 : 3 – 7. 🕮 **Soma** mistari yenye Mkushi alikuwa akisoma.

Filipo aliuliza Mkushi, "Unaelewa chenye unasoma?" Alimjibu, "Nitaelewaje kama mtu hajanielezea?" Mkushi alimkaribisha Filipo apande juu ya gari na wakae wote. Aliuliza Filipo, "Niambie, huyu nabii anazungumza juu ya nani? Anazungumza juu yake mwenyewe au juu ya mtu mwingine?"

Filipo alikaa na Mkushi kwa gari lake. Waliendelea wote pamoja. Filipo alifundisha Mkushi kuhusu Yesu. Alimwonyesha mistari mingi sana kwa Agano la Kale zenye zinazungumza habari ya Yesu. Filipo alimwambia vile Yesu alitimiza ahadi za Mungu kwa Agano la Kale. Filipo alimwambia kwamba Yesu alitupenda sisi wote sana hata akafa msalabani kwa ajili yetu. Tukimpenda na tumtii, tutaishi milele kwa Ufalme wa Mungu.Filipo alimwambia kwamba, Yesu anataka tujute dhambi zetu. Yesu anataka tubatizwe ili tusamehewe dhambi zetu. Yesu anataka tubatizwe ili tuishi maisha mapya tukimtumkia.

Mkushi alifurahi sana aliposikia hizo Habari Njema. Alifurahi kusikia juu ya Yesu na upendo wake kwetu. Alifurahi aliposikia juu ya Ufalme wa Mungu wa ajabu wenye Yesu atakuja kusimamisha hapa duniani atakaporudi.

Filipo na Mkushi walipokuwa wakiendelea na safari, waliona maji kando. Mkushi alisema, "Angalia hapa kuna maji. Ninaweza kubatizwa?" Filipo alimjibu Mkushi, "Ikiwa unaamini na moyo wako wote, unaweza kubatizwa?" Mkushi alijibu, "Ninaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu."

Mkushi alisimamisha gari. Filipo na Mkushi walitelemka na kuenda ndani ya maji. Filipo alimbatiza Mkushi kwa kumweka mpaka ndani ya maji. Halafu wote wawili walitoka ndani ya maji. Filipo akatoka na kwenda zake. Mkushi aliendelea na safari yake akiwa na furaha.

